Viwango vya kujifunza na kutahini katika Jimbo

"Viwango vya kujifunza" ni nini?

'Viwango vya kujifunza' vya Jimbo la Washington K-12 hufafanua ni nini wanafunzi wote wanapaswa kujua na kuwa na uwezo wa kufanya katika kila darasa.

Kwa nini tunavihitaji?

Viwango vya elimu ya ukali zinahitaji wanafunzi kufikiri kwa umakinifu na ubunifu kuhusu maudhui—badala ya kukariri—hivyo wao wako tayari kwa ajili ya kazi, chuo, na maisha baada ya shule ya sekondari.

Maudhui na maeneo ambayo yana viwango vya kujifunza ni yapi?

- Lugha ya Kiingereza Sanaa
- Hisabati
- Sayansi
- Mafunzo ya Jamii
- Sanaa
- Teknolojia ya Elimu
- Afya na hali nzuri ya mwili
- Jumuishi ya mazingira na uendelevu
- Lugha za dunia
- Ustadi wa lugha ya Kiingereza

Vinaendelezwa namna gani?

Viwango vya kujifunza vinaendelezwa kwa makini na wataalamu wa maudhui kutoka katika jimbo hilo na taifa, na pembejeo kutoka waelimishaji, wazazi, na umma.

Viwango vya kujifunzia huboreshwa mara ngapi?

Viwango hivi vinaboreshwa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa vinalingana na matarajio ya vyuo na kazi.

Kwa nini tuna mitihani ya jimbo?

Data ya mafanikio ya wanafunzi, shule, wilaya, na jimbo huwasaidia waelimishaji kuboresha ufundishaji. Alama za mitihani huwasaidia kuamua ni desturi na raslimali gani za ufundishaji zinazosaidia zaidi uelewaji wa mwanafunzi wa viwango vya kujifunza. Alama hizo hutumiwa kuboresha ufundishaji. Matokeo hayo hutambua pale ambapo wanafunzi wanafanya vyema na pale ambapo wanahitaji usaidizi wa ziada ili waweze kutimiza matarajio ya darasa.

Pia, alama za watoto huzipa familia taarifa muhimu kuhusu jinsi mtoto wao anavyoendelea na pale ambapo usaidizi wa ziada unahitajika.

Mitihani inayohusisha jimbo lote ni muhimu kwa sababu huwa inasaidia kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wa shule za umma, bila kujali wanakoenda shule, wanapata elimu bora.

Je Zinahitajika?

Jimbo na sheria za shirikisho zinahitaji wanafunzi kutahiniwa katika:

- **Sanaa ya lugha ya Kiingereza na hisabati:** Wanafunzi wa darasa 3 hadi ya 8 na shule ya sekondari
- **Sayansi:** Wanafunzi wa darasa: 5, 8, na 10

Kuona mitihani gani inahitajika ili kuhitimu shule ya sekondari, tafadhali tembelea www.WAtesting.com.

Kujifunza zaidi!

Viwango Kujifunza

bit.ly/StateStandards
au barua pepe CoreStandards@k12.wa.us

Kujifunza zaidi!

Mitihani ya jimbo

www.WAtesting.com
au barua pepe StateTesting@k12.wa.us

Viwango vya Kujifunza na Kutahini katika Jimbo

KWELI 10 BORA KUHUSU VIWANGO VYA KUJIFUNZA VYA K-12 VYA WASHINGTON NA TATHMINI

Sababu #1

Mambo sahihi

Viwango vya kujifunza vya jimbo la Washington katika sanaa za lugha ya Kiingereza na hisabati, na tathmini zilizopangwa za Smarter Balanced, zimeundwa kwa minajili ya kuwatayarisha wanafunzi kwa chuo, kazi na maisha.

Sababu #2

Stadi za ulimwengu halisi

Viwango na tathmini hizi huangazia stadi za ulimwengu halisi kama utatuzi wa matatizo, kufikiri kimakinifu na kuandika. Wanafunzi huombwa kufanya mengi zaidi kuliko kujaza viputo kwenye mtihani ulio na machaguo mengi. Sasa wana nafasi ya kuonyesha kazi yao, kuandika na kueleza majibu yao kama sehemu ya mchakato wa kutahiniwa.

Sababu #3

Unahusiana na darasa

Mtihani huu unalingana na stadi na maudhui ambayo wanafunzi wanasoma na kufanyia mazoezi darasani kila siku. Kila darasa lina malengo wazi yaliyopewa kipaumbele yanayofafanua kile ambacho wanafunzi wanapaswa kujua na kuelewa, mwishoni mwa mwaka unapofika.

Sababu #4

Kuziba nyufa

Tathmini hizi husaidia kutambua nyufa za mafanikio na huruhusu mamlaka ya wilaya za shule na jimbo kuweka raslimali zinapohitajika kabisa.

Sababu #5

Mitihani ni mbinu moja tu

Mitihani ya jimbo ni mojawapo kati ya viashirio kadhaa, pamoja na kadi ya ripoti, maoni ya mwalimu na kazi za darasani vinavyotumiwa kuundia taswira kamili ya maendeleo ya mwanafunzi shuleni.

Sababu #6

Uhusiano na elimu ya juu

Vyuo vikuu, vyuo na vyuo vya jamii vya Washington hutumia alama za Smarter Balanced za wanafunzi wa shule za sekondari kuwachagua kwa kozi fulani.

Sababu #7

Raslimali za mwelimishaji

Kwa kutumia mfumo wa kutathmini wa Smarter Balanced, waalimu wanaweza kupata rasilimali katika maktaba ya dijitali na kisha kutumia tathmini za mara kwa mara, au za muda mfupi, kufuatilia na kusaidia maendeleo ya wanafunzi katika mwaka mzima.

Sababu #8

Kuhusishwa kwa walimu

Walimu wa Washington wamehusishwa katika kila hatua ya kuunda mfumo wa kutathmini wa Smarter Balanced, kuanzia kuunda vipengee vya tathmini, hadi kuweka viwango vya mafanikio, hadi kuchunguza raslimali za maktaba ya dijitali.

Sababu #9

Matokeo ya haraka

Katika majira ya machipuko mwaka wa 2016, alama za mitihani za wanafunzi binafsi zilikuwa zinapatikana kwenye mamlaka ya wilaya ndani ya wiki mbili hadi tatu baada ya wanafunzi kukamilisha mitihani yao ya mwisho wa mwaka, au mitihani inayoangazia matokeo ya ujumla. Hii husaidia walimu kuboresha ufundishaji.

Sababu #10

Inapatikana kwa wengi

Mitihani ya Smarter Balanced imeundwa kuwashughulikia wanafunzi wote, ikiwa ni pamoja na wale wenye ulemavu na wanafunzi wa lugha ya Kiingereza.